

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**KIKAO CHA ISHIRINI NA SABA**

**17 MEI, 2023**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**KIKAO CHA ISHIRINI NA SABA– TAREHE 17 MEI, 2023**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**III. MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**347. MHESHIMIWA ASHA ABDULLAH JUMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwawezesha kimaendeleo Vijana wa Skauti Nchini.

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**348. MHESHIMIWA DANIEL BARAN SILLO (BABATI VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapunguza tatizo la upungufu wa Walimu katika Shule za Sekondari Babati Vijijini.

**349. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINA CHRISTOPHER MNZAVA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaipandisha hadhi Zahanati ya Solwa kuwa Kituo cha Afya.

**350. MHESHIMIWA DEO KASENYENDA SANGA (MAKAMBAKO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaowaongezea posho Madiwani.

**351. MHESHIMIWA EMMANUEL ADAMSON MWAKASAKA (TABORA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatatua changamoto ya ukosefu wa Vituo vya Afya katika Jimbo la Tabora Mjini.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**352. MHESHIMIWA ANGELINA ADAM MALEMBEKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, ni changamoto gani mpya za Muungano zimejitokeza.

**353. MHESHIMIWA ZAHOR MOHAMMED HAJI (MWERA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, kwa nini Halmashauri ya Magharibi 'A' imeweka Sheria ya Kodi na VAT kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**354. MHESHIMIWA DANIEL AWACK TLEMAI (KARATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya ujenzi wa barabara ya Matala - Mwanhuzi - Lalago kwa kiwango cha lami.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**355. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA (URAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini majengo yataongezwa katika Chuo cha VETA Urambo ili kuongeza fani ambazo hazitolewi kwa sasa.



**356. MHESHIMIWA NAGHENJWA LIVINGSTONE KABOYOKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuanzisha masomo yatakayoibua vipaji vya Watoto kuanzia Shule za Msingi.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**357. MHESHIMIWA ANTIPAS ZENO MGUNGUSI (MALINYI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini *UCSAF* itapeleka minara ya mawasiliano Wilaya ya Malinyi kwani maeneo mengi hayana mawasiliano.

**WIZARA YA KILIMO:**

**358. MHESHIMIWA SHABAN OMARI SHEKILINDI (LUSHOTO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua zao la Kahawa Wilayani Lushoto.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**359. MHESHIMIWA HAJI MAKAME MLENGE (CHWAKA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini warithi wa Askari E2152 aliyekuwa Mtumishi wa Jeshi la Polisi watapewa Mafao yao.

**360. MHESHIMIWA DOROTHY GEORGE KILAVE (TEMEKE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, nini tamko la Serikali kuhusu Kitambulisho cha Taifa kuwekwa ukomo wa kutumika.

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

**361. MHESHIMIWA ENG. MWANAISHA NG'ANZI ULENGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, lini Serikali itawahamisha Wataalam wa Maendeleo ya Jamii kuwa chini ya Wizara.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

##### **WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**DODOMA  
17 MEI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**